Nation Media Group
Media of Africa for Africa

www.nationmedia.com
Nation Media Group | Nationmediagroup | @NationMediaGrp

# SHIRIKA LA NATION MEDIA

(Imesajiliwa Kenya chini ya Sheria ya Makampuni)
(Nambari ya Usajili 85/74)

## TAARIFA KUHUSU MKUTANO MKUU WA KILA MWAKA

Taarifa imetolewa hapa kwamba Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa Sitini na Moja wa Wenyehisa wa Shirika la Nation Media Group PLC utafanyika mtandaoni siku ya Ijumaa, tarehe 28 Juni 2024 saa 9.00 jioni Saa za Afrika Mashariki ili kuendesha shughuli zilizotajwa hapo chini.

*Maamuzi yote yataendeshwa kupitia Kura ya maoni.*

**SHUGHULI YA KAWAIDA**

**1.** Kupokea taarifa za kifedha za mwaka uliokamilika tarehe 31 Disemba 2023, na ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi na Wakaguzi.

**2.** Kuangazia kuwa Wakurugenzi hawapendekezi mgawo wa hisa kwa mwaka uliokamilisha tarehe 31 Disemba 2023.

**3.** Kupokea, kuzingatia na ikifikiri kuwa ni sawa, iidhinishe Ripoti ya Mshahara wa Wakurugenzi na mshahara uliolipwa kwa Wakurugenzi kwa mwaka uliokamilika tarehe 31 Disemba 2023 na kuidhinisha Bodi kurekebisha mshahara wa Wakurugenzi Wasio Watendaji.

**4.** Kuthibitishia Wakaguzi kwamba kampuni ya PricewaterhouseCoopers LLP, baada ya kuonyesha nia yake, itaendelea kuhudumu kama Mkaguzi wa Kampuni kwa mujibu wa kifungu cha 721(2) cha Sheria ya Kampuni ya Kenya 2015 na kuidhinisha Wakurugenzi kurekebisha mshahara wa Wakaguzi.

**5.** Kuchagua tena Wakurugenzi watendaji:
- a) Bw. Sultan Allana aliteuliwa mnamo tarehe 2 Mei 2024 kuchukua nafasi ya kawaida na kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Makala ya Muundo wa Kampuni, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ili kuchaguliwa tena;
- b) Bw. Fayyaz Nurmohamed aliteuliwa mnamo tarehe 2 Mei 2024 kuchukua nafasi ya kawaida na kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Makala ya Muundo wa Kampuni, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ili kuchaguliwa tena;
- c) Bi. Nancy Matimu aliteuliwa mnamo tarehe 2 Mei 2024 kuchukua nafasi ya kawaida na kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Makala ya Muundo wa Kampuni, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ili kuchaguliwa tena;
- d) kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Taarifa ya Ushirika ya Kampuni, Bi. Sumayya Hassan, anastaafu kwa mzunguko na hajajitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
- e) kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Taarifa ya Ushirika ya Kampuni, Bw. Dennis Aluanga, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
- f) kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Taarifa ya Ushirika ya Kampuni, Prof. Samuel Sejjaaka, anastaafu kwa mzunguko na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
- g) Dkt. Wilfred Kiboro, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
- h) Bw. Francis O. Okello, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na hajajitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
- i) Dkt. Yasmin Jetha, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
- j) Bw. Wangethi Mwangi, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na hajajitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
- k) Bw. Leonard Mususa, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;

**6.** Kuteua wanachama wa Kamati ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu ya Kampuni:

Kwa mujibu wa kifungu cha 769(1) cha Sheria ya Kampuni ya 2015, Wakurugenzi wafuatao kwa kuwa wanachama wa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu wachaguliwe tena ili kuendelea kuhudumu kama wanachama wa Kamati iliyotajwa:

- a) Bw. Leonard Mususa
- b) Bw. Al-Noor Ramji
- c) Prof. Samuel Sejjaaka
- d) Dkt. Yasmin Jetha

**SHUGHULI MAALUM**

**7.** Shughuli nyingine yoyote ambayo Taarifa yake halali imetolewa.

**Kwa Agizo la Bodi**

Angela Namwakira
Katibu wa Kampuni

Tarehe 6 Juni 2024

**VIDOKEZO:**

1. Kwa mujibu wa vipengee vya sehemu ya 3 ya Sheria ya Kampuni hiyo, 2015, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Biashara (Marekebisho) (Nambari 2), 2021, Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa Sitini na Moja (AGM) wa Shirika la NATION MEDIA GROUP PLC ("Kampuni hiyo") utafanywa mtandaoni siku ya Alhamisi, tarehe 28 Juni 2024 saa 9.00 jioni.

2. Wenyehisa wote watasajiliwa mapema kwa kutumia maelezo yao ya data pepe kwenye Sajili ya Kampuni na watapokea kiungo cha kibinafsi kupitia SMS na/au baruapepe Wenyehisa ambao wangependa kushiriki katika mkutano bado wanapaswa kuthibitisha kuwa watahudhuria kupitia USSD kwa kutumia namba fupi *483*102# au kupitia kiungo cha Mfumo wa AGM ambacho watatumiwa kupitia SMS na/au baruapepe au kupitia https://digital.candrgroup.co.ke na kufuata maelekezo mbalimbali kuhusiana na mchakato wa kujisajili. Ili kukamilisha mchakato wa kujisajili, wenyehisa ambao hawatumii kiungo cha kujisajili mapema watahitaji kuwa tayari na Nambari zao za Vitambulisho/Pasipoti zilizotumiwa kununua hisa zao na nambari za Akaunti zao za CDSC.

3. Shughuli ya kujisajili kwa AGM itaanza tarehe 10 Juni 2024 saa 03:00 asubuhi na itafungwa tarehe 27 Juni 2024 saa 6 Adhuhuri.

4. Ili kupata usaidizi, wenyehisa wanapaswa kupiga nambari zifuatazo za usaidizi: +254 20 8690360 kuanzia 2:00 asubuhi. hadi 10:00 jioni. wakati ujisajili unaendelea. Wenyehisa wowote walio nje ya Kenya wanapaswa kupiga nambari ya usaidizi ili wasaidiwe kujisajili au watume baruapepe kwa digital@candrgroup.co.ke.

5. Kwa mujibu wa Sehemu ya 283 (2) (c) ya Shria ya Kampuni, hati zifuatazo zinaweza kutazamwa kwenye tovuti ya Kampuni kupitia https://www.nationmedia.com
   - a. nakala ya Taarifa hii na Fomu ya Mshirika;
   - b. Taarifa za Kifedha Zilizokaguliwa za Kampuni za mwaka uliokamilika tarehe 31 Disemba 2023;

6. Wenyehisa ambao wangependa kuuliza maswali yoyote kwa ajili ya AGM wanaweza kufanya hivyo kwa:
   - (i) Kutumia kiungo kilichotolewa kupitia sms/baruapepe baada ya kuthibitisha usajili; au
   - (ii) Ili kufikia AGM Inayofanyika Mtandaoni kupitia https://digital.candrgroup.co.ke au kupitia kiungo cha mfumo wa AGM; Chagua Hudhuria Tukio; Chagua kichupo cha chaguo la "Q&A" na uwasilishe maswali kwenye kisanduku cha matini; au
   - (iii) Kufikia AGM Inayofanyika Mtandaoni kupitia mfumo wa USSD *483*102#; Tumia vidokezo vya menyu ili Uchague chaguo la "Q&A" na watume maswali yao (kwa herufi zisizozidi 160 za matini ya sms); au
   - (iv) Kutuma maswali yao yaliyoandikwa kupitia baruapepe kwenda digital@candrgoup.co.ke; au
   - (v) Kadiri inavyowezekana, kuwasilisha maswali yao yaliyaondikwa wao wenyewe mahali halisi pa kutuma au anwani ya baruapepe kwa ofisi ya Custody and Registrars Services Ltd, Wasajili wa Kampuni, katika Jumba la IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1, Barabara ya 5th Ngong. Wenyehisa wanaotuma maswali kupitia baruapepe au kuwasilisha kwa C&R Group ni sharti watoe maelezo yao kikamilifu (majina kamili, Nambari ya Akaunti ya Hisa//Nambari ya Akaunti ya CDSC) wanapotuma maswali na ufafanuzi wao. Pia ambatanisha nakala ya Kitambulisho/Pasipoti yako.

   **Maswali kupitia kituo cha AGM**
   Wenyehisa wataweza kuuliza maswali kwenye mfumo wa mtandaoni wa AGM hadi na wakati wa AGM wakitumia kituo cha mtandaoni au msimbo wa USSD.

   **Maswali Mubashara wakati wa AGM**
   Fursa itatolewa kwa wenyehisa kujiunga kwenye AGM mtandaoni ili kuuliza maswali yao wakati wa mkutano. Wenyehisa ambao wangependa kuuliza maswali yao mubashara wakati AGM ikiendelea wanaweza kujiunga chumba cha mkutano mtandaoni wakati wa AGM (kwa kuchagua kichupo cha "Jiunge kwenye Chumba cha Mkutano wa AGM" katika sehemu ya chini ya dirisha linaloonyesha mtiririko mubashara). Katika chumba cha mkutano, wenyehisa wanaweza kuendelea kutazama tangazo la AGM na ama i) kuchagua chaguo la "inua mkono" kwenye skrini yao ili kuomba fursa ya kuuliza maswali yao moja kwa moja kwa Bodi au ii) kuweka maswali yao kwenye gumzo mubashara ili yasomwe kwa sauti kwa Bodi wakati wa AGM.

7. Wenyehisa ambao wangependa kupiga kura wanaweza kufanya hivyo kwa:
   - (i) Kufikia AGM Mtandaoni https://digital.candrgroup.co.ke au kupitia kiungo cha mfumo wa AGM; Chagua Hudhuria Mkutano; Chagua kichupo cha chaguo la "Kupiga kura" na upige kura; au
   - (ii) Kufikia AGM Mtandaoni kupitia mfumo wa USSD kwa kubofya *483*102#; Tumia vidokezo kwenye menyu Kuchagua chaguo la "Kupiga kura" na kufuata vidokezo kadhaa kuhusiana na mchakato wa kupiga kura.

8. Kwa mujibu wa Sehemu ya 298(1) ya Sheria ya Kampuni, wenyehisa walio na haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika AGM wana haki ya kuteua mshirika kupiga kura kwa niaba yao. Si lazima mshirika awe mwanachama wa Kampuni lakini asipokuwa Mwenyekiti wa AGM. Fomu ya mshirika imeambatanishwa kwenye Taarifa hii na inapatikana kwenye wavuti wa Kampuni https://www.nationmedia.com. Nakala halisi za fomu ya mshirika pia zinapatikana mahali yafuatayo:

   **Ofisi za Custody and Registrars Services,**
   **IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1,**
   **Barabara ya 5th Ngong.**

   Ili iwe sahihi, fomu ya mshirika lazima ijazwe na mwenyehisa au wakili wake ambaye amehalalishwa kupitia maandishi. Ikiwa mwenyehisa ni shirika, chombo kinachoteua mshirika kitatolewa chini ya muhuri ya kawaida (ikiwa ipo) au chini ya mkono wa afisa au wakili aliyehalalishwa wa shirika kama hilo.
   Fomu ya mshirika iliyojazwa inapaswa kutumwa kupitia baruapepe kwa proxy@candrgroup.co.ke katika muundo wa pdf na kuwasilishwa kwa Custody and Registrars Services, IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1, Barabara ya 5th Ngong Nairobi au itumwe kupitia barua posta kwa Custody and Registrars Services, S.L.P 8484-00100 Nairobi ili ifikie kwa Msajili au Katibu wa Kampuni ifikapo saa 9.00 jioni, tarehe 26 Juni 2024.
   Fomu zilizojazwa lazima ziambatanishwa na nakala ya Kitambulisho/Pasipoti halali ya mwanachama na kujumuisha Kitambulisho/Pasipoti, baruapepe au nambari ya simu ya mshirika huyo ili kuwezesha mchakato wa usajili. Mawasiliano kuhusu usajili wowote wa mshirika utakaokataliwa yatatolewa kwa mwenyehisa husika mwisho tarehe 29 Juni, 2024 saa 9.00 jioni ili kuruhusu muda wa kutatua masuala.

9. Mkutano wa AGM utaririshwa moja kwa moja kwa wenyehisa wote ambao watakuwa wamejisajili kushiriki katika mkutano.

10. Wenyehisa waliosajiliwa na washirika wao watapokea ujumbe wa SMS/ na/au baruapepe saa mbili kabla ya AGM, ikiwakumbusha wenyehisa waliosajiliwa na washiria wao kwamba AGM itaanza baada ya saa Mbili na kutoa kiungo cha kutiririsha moja kwa moja.

11. Wenyehisa na washirika waliosajiliwa wanaweza kupiga kura (Mwenyekiti akiwaomba kufanya hivyo) kupitia USSD *483*102# au kwenye Mfumo wa AGM.

12. Kura ya maoni itapigwa kwa maamuzi yote yatakayowasilishwa kwenye taarifa.

13. Matokeo ya AGM yatachapishwa kwenye wavuti wa kampuni (www.nationmedia.com) ndani ya saa 24 baada ya kutamatika kwa AGM.

Kwa migao ya hisa ambayo haijadaiwa, mbinu inayopendekezwa ya kulipa migao ya hisa ambayo ni chini ya Kshs 200,000 ni kupitia M-PESA. Wenyehisa ambao wangependa kupokea mgao wao kupitia M-PESA na hawajisajili katika njia hii ya malipo wanaweza kuchagua kupokea migao ya siku zijazo kwa kubonyeza *483*038# au kuwasiliana na Share Registrar, Custody & Registrars Services Limited.
Wenyehisa wote wa sasa na wa zamani wa Kampuni wanaarifiwa hapa kwamba kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya Mali za Kifedha ambazo Hazijadaiwa No 40 ya 2011 Sehemu ya II na III, migao na hisa ambazo hazijadaiwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) au zaidi zitahitaji kuwasilishwa kwa Mamlaka Inayoshughulikia Mali ya Kifedha ambayo Haijadaiwa ('Mamlaka hiyo') kama mali iliyotelekezwa katika tarehe iliyoteuliwa.
Kwa hiyo, wenyehisa wote wa sasa na wa zamani ambao wana migao ambayo hajalipwa wanahitajika kuwasiliana na Share Registrar, Custody & Registrars Services Limited kupitia anwani iliyoashiriwa hapo chini ili kudai migao yoyote ambayo haijalipwa ili kuepuka hatari ya migao kupekelekwa kwa Mamlaka.

**Custody and Registrars Services Ltd (C&R Group),**
**IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1,**
**Barabara ya 5th Ngong, Nairobi,**
**Simu + 254 20 760 8216.**

OUR BRANDS